MAMLAKA YA HALI YA HEWA TANZANIA



JARIDA LA HALI YA HEWA KILIMO

*Na.2. Msimu wa Kilimo 2023/24*    *Tathmini ya Oktoba 11-20, 2023 na Matazamio kwa Kipindi cha Oktoba 21-31, 2023*

**MUHTASARI**

- Mvua zinazotarajiwa katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi na pwani ya kaskazini zinatarajiwa kuongeza unyevunyevu katika udongo
- Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Vuli wanashauriwa kuendelea na shughuli za kuandaa mashamba kupanda pale wanapoona unyevu wa udongo unatosha mbegu kuota


## MIFUMO YA HALI YA HEWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2023

Kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia (St. Helena na Mascarene) iliendelea kupungua wakati ile iliyopo kaskazini mwa dunia (Azore na Siberia) iliendelea kuimarika. Hali hii iliendelea kuimarisha ukanda mvua (ITCZ) kuwepo katika maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria na magharibi mwa nchi.

Joto la bahari la juu kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto la bahari la chini kidogo ya wastani liliendelea kuwepo katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi, hali hii ilichangia katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuvuma kutoka baharini kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani hususani katika nusu ya pili ya dekadi.

## TATHMINI YA MVUA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2023

Katika kipindi hicho, maeneo mengi nchini yalipata mvua nyepesi ikiwemo baadhi ya maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria, magharibi, ukanda wa Pwani ambayo yalipata jumla ya mvua kwa siku 10 kati ya milimita 11 mpaka 100. Hata hivyo, maeneo machache ya mkoa wa Tanga yalipata mvua zaidi ya milimita 150 kama inavyoonekana katika kielelezo.




Kielelezo: Kiasi cha mvua cha Oktoba 11-20, 2023 kama kilivyokadiriwa na satellite (RFE)

## TATHMINI YA HALI YA KILIMO KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2023

Katika dikadi hii, mvua zilizonyesha zilisaidia ongezeko la unyevunyevu kwenye udongo katika baadhi ya maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi, pwani ya kaskazini (hususan mkoa wa Tanga na kaskazini mwa Morogoro) kwa shughuli za upandaji wa mazao.

Kwa ujumla, katika maeneo yanayopata mvua za vuli, wakulima waliendelea na uandaaji wa mashamba na upandaji wa mazao isipokuwa katika mkoa wa Kagera ambako mahindi yapo katika hatua ya ukuaji na wakulima wanaendelea na palizi.

Upatikanaji wa maji na malisho kwa ajili ya mifugo na wanyama pori ulipungua katika maeneo mengi nchini hususani maeneo yanayopata

mvua mara moja kwa mwaka kutokana na hali ya ukavu wa muda mrefu.

## HALI YA MAJI KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 11-20, 2023

Kwa ujumla kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vimeendelea kupungua katika mabonde mengi nchini kutokana hali ya ukavu ya muda mrefu.

## MIFUMO YA HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2023

Katika kipindi hiki, migandamizo mikubwa ya hewa iliyopo kusini mwa dunia inatarajiwa kuendelea kupungua nguvu wakati ile iliyopo katika kizio cha kaskazini inatarajiwa kuendelea kuimarika. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuimarisha ukanda mvua (ITCZ) kuwepo katika maeneo ya ukanda wa ziwa Victoria na magharibi mwa nchi.

Joto la bahari la juu kidogo ya wastani linatarajiwa kuendelea katika eneo la magharibi mwa bahari ya Hindi wakati joto la bahari la chini kidogo ya wastani linatarajiwa katika eneo la mashariki mwa bahari ya Hindi. Hali hii inatarajiwa kuendelea kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kuelekea katika maeneo ya ukanda wa pwani.
Joto la bahari katika eneo la kusini mashariki mwa bahari ya Atlantiki (karibu na pwani ya Angola) linatarajiwa kuwa la wastani hadi juu ya wastani na hivyo kuwa na mchango mdogo katika kuusukuma upepo wenye unyevunyevu kutoka misitu ya Congo kuelekea magharibi mwa nchi.

## HALI YA HEWA INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2023

Maeneo ya ukanda wa Ziwa Victoria (mikoa ya Kagera, Geita, Shinyanga, Mwanza, Simiyu na Mara) na magharibi mwa nchi (mikoa ya Kigoma, Katavi na Tabora) yanatarajiwa kuwa na mvua pamoja na ngurumo za radi katika baadhi ya maeneo.

Pwani ya kaskazini (mikoa ya Tanga, maeneo ya kaskazini mwa Morogoro, Pwani na Dar es Salaam vikiwemo visiwa vya Unguja na Pemba) pamoja na nyanda za juu kaskazini mashariki (mikoa ya Arusha, Manyara na Kilimanjaro) inatarajiwa kuwa na mvua katika baadhi ya maeneo.

Maeneo ya pwani ya kusini (mikoa ya Mtwara na Lindi) na nyanda za juu kusini magharibi (mikoa ya Rukwa, Songwe, Mbeya, Njombe na Iringa) yanatarajiwa kuwa na vipindi vya mvua nyepesi katika maeneo machache.

Kanda ya kati (mikoa ya Dodoma na Singida) na kanda ya kusini (mkoa wa Ruvuma na maeneo ya kusini mwa Morogoro) maeneo hayo yanatarajiwa kuwa na vipindi vya ukavu.

## HALI YA HEWA KILIMO: MATARAJIO NA USHAURI KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2023

Mvua inayotarajiwa hususan katika maeneo ya kanda ya Ziwa Victoria, magharibi mwa nchi na pwani ya kaskazini zitasaidia kuongeza unyevunyevu katika udongo na ukuaji wa mazao.

Wakulima katika maeneo yanayopata mvua za Vuli hususan pwani ya kaskazini na nyanda za juu kaskazini wanashauriwa kuendelea na kupanda mazao pale wanapoona unyevunyevu wa udongo unatosha mbegu kuota.

Wavuvi wanashauriwa kuendelea kufuatilia taarifa za hali ya hewa za kila siku, hususan kwenye bahari ya Hindi na maziwa makuu ili kufanya maamuzi juu ya wakati sahihi wa kwenda kufanya shughuli za uvuvi kutokana na hali ya upepo inayojitokeza mara kwa mara.

Kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa katika maeneo mengi nchini, wafugaji wanashauriwa kutumia maji na malisho yaliyopo kwa uangalifu.

## HALI YA MAJI INAYOTARAJIWA KATIKA KIPINDI CHA OKTOBA 21-31, 2023

Kina cha maji katika mabwawa na mtiririko wa maji kwenye mito vinatarajiwa kuendelea kupungua kutokana na hali ya ukavu inayotarajiwa hususan katika maeneo yanayopata msimu mmoja wa mvua. Jamii inashauriwa kuendelea kutumia maji yaliyopo kwa uangalifu kufuatia kuendelea kwa msimu wa ukavu katika maeneo mengi nchini.

Jengo la Utawala, Ndaki ya Sayansi za Kompyuta na Elimu Angavu, Chuo Kikuu cha Dodoma,
1 Mtaa wa CIVE, S.L.P 27, 41218 Dodoma, Simu: +255 26 2962610, Nukushi: +255 26 2962610,
Barua pepe: met@meteo.go.tz; agromet@meteo.go.tz; Tovuti: www.meteo.go.tz
(ISO 9001:2015 Certified in Aviation Services)